

## Kuhusu Mwandishi

### Allamah Syed Murtadha Askari

Allamah Syed Murtadha Askari ni mwanazuoni wa Shia'h anayetambulika, ambaye vitabu vyake katika historia ya Kiislamu, masomo yanayowiana ya madhehebu mbalimbali ndani ya jamii ya Uislamu na falsafa, vimeacha alama isiyofutika.

Kwenye kutambulika heshima yake kuna vitabu vikubwa kama “Abdullah ibn Saba,” “Masahaba wa Mtume (s.a..w.w.) 150 wa bandia,” na kile “Sifa bainifu za kawaida za madhehebu mbili (za Kiislamu).” Baadhi ya uchambuzi wa awali na uchunguzi wa kisayansi katika nyanja ya historia ya Kiislamu umevunja zile fikra na mawazo yaliyokuwa yamekubalika hadi sasa, na kusababisha makelele yasiyo na kifani, ambayo hayajawahi kutokea miongoni mwa washikilia elimu ya vitabuni wasiobadilika na wenye imani kamili ya dunia ya Kiislamu.

Kama mwanaharakati wa kisiasa, Allamah anafahamika kwa maoni yake thabiti na mapambano juu ya kuhuisha Uislamu. Wengi wa marafiki zake na washirika wake wameuawa kishahidi na utawala katili wa Iraq. Allamah yuko juu sana miongoni mwa wanazuoni wakubwa wanaoweza kusimama kutokana na makumbusho ya nyuma ya mapambano makali dhidi ya uasi wa kujitokeza kwa Wa-Ba'th. Yeye ni mzungumzaji mwenye mvuto na muongeeji mcheshi; na hata katika umri wa zaidi ya miaka themanini, haonyeshi dalili yoyote ya kudhoofika kwa raghba!

Mwenyezi Mungu amdumishe zaidi!